

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO  
SHULE YA SEKONDARI MAZOMBE, S. L. P 105, MAZOMBE**

**Kumb. Na. MAZOSS/JOIN/2021/134**

KWA MWANAFUNZI .....

K.K. MZAZI/MLEZI WA

MWANAFUNZI.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAZOMBE MWAKA  
2021.**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Mazombe baada ya kuwa umefanya vizuri na kufaulu mitihani ya darasa la saba mwaka 2020. Nakupongeza sana.

Shule ya Sekondari Mazombe ni shule iliyopo wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa katika kijiji cha Mazombe umbali wa kilomita mbili (2) kutoka barabara kuu iendayo Dar es salaam. Shule imesajiliwa kwa namba S.3408. Shule ni mchanganyiko, yaani wavulana na wasichana na ni shule ya kutwa, wanafunzi wote hukaa katika makazi yao ya nje ya shule. Aidha, shule ina Hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike tu kwa wale wanaohitaji.

Masomo ya muhula wa kwanza mwaka 2020 yanaanza rasmi tarehe **11/01/2021. WANAFUNZI  
WOTE WANATAKIWA KURIPOTI SHULENI TAREHE HIYO BILA KUKOSA**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1. SARE YA SHULE**

**A. WAVULANA**

- i Mashati mawili meupe yenyе mikono mifupi.
- ii Suruali mbili rangi ya kijivu zinzaokubalika (zisizochongwa).
- iii Sweta rangi ya kijani lenye (V) shingoni.
- iv Viatu jozi mbili au zaidi nyeusi, vyenye visigino vifupi, vya Kamba.
- v Soksi jozi mbili au zaidi rangi nyeupe.
- vi Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
- vii Nguo za michezo.

**B. WASICHANA**

- i Mashati mawili meupe yenyе mikono mifupi.
- ii Sketi mbili rangi ya kijivu zinazopita magoti.
- iii Sweta rangi ya kijani lenye (V) shingoni.
- iv Viatu jozi mbili au zaidi nyeusi vyenye visigino vifupi vya Kamba.

- v Soksi jozi mbili au zaidi rangi nyeupe.
- vi Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
- vii Nguo za michezo.

### C. WASICHANA WAISLAMU

- i Shati nusu kanzu rangi nyeupe mikono mirefu.
- ii Suruali rangi ya kijivu inayokubalika
- iii Sweta rangi ya kijani lenye (V) shingoni.
- iv Viatu jozi mbili au zaidi nyeusi vyenye visigino vifupi nya kamba.
- v Soksi jozi mbili au zaidi rangi nyeupe.
- vi Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
- vii Tracksuit kwa ajili ya michezo.
- viii Hijab rangi nyeupe.

### 2. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA SHULE

- i Daftari kubwa zisizopungua 12
- ii Vifaa nya Hisabati: Mkebe, Rula, Graph pad, Mathematical table (four figure)
- iii Faili la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi**
- iv Jembe moja lenye mpini (atacaa nalo nyumbani)
- v Ndoo moja ya lita kumi (atacaa nayo nyumbani)
- vi Fyekeo moja (atacaa nalo nyumbani)
- vii **VITABU:** Tunashauri mzazi/mlezi umnunulie mwanaao vitabu nya kutosha baada ya kushauriana na mwalimu.

### 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha, shule inazingatia miongozo inayotolewa na wizara inayohusika na masuala ya elimu nchini. Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo akiwa shulenii na nyumbani.

- (a) Heshima kwa viongozi, walimu na wafanyakazi, wazazi, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri kwa kila siku awapo darasani na shughuli zote za ndani nan je ya shule.
- (c) Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wa shule muda wote ni jambo la lazima.
- (d) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule ni jambo la lazima.
- (e) Kutunza mali za shule ni lazima.
- (f) Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (h) Kuwahi katika shughuli za shule na nyinezo unazopewa.
- (i) Kutimiza maandalio ya jioni pale yanapotolewa.
- (j) Mwanafunzi **haruhusiwi** kuwa au kumiliki simu akiwa shulenii na nyumbani.

#### **4. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

- (a). Wizi mdogo na mkubwa
- (b). Uasherati, ubakaji na ushoga
- (c). Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- (d). Uvutaji bangi
- (e). Makosa ya jinai
- (f). Kupiga na kupigana
- (g). Kuharibu mali ya umma
- (h). Kudharau Bendera ya Taifa
- (i). Kuoa au kuolewa
- (j). Kupata mimba au kusababisha mimba ndani nan je ya shule
- (k). Kutoa mimba
- (l). Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo pamoja na kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
- (m). Kukataa adhabu kwa makusudi

#### **5. MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA**

- i **Uongozi wa shule unaagiza kuwa wanafunzi wote hawatakiwi kukaa nje ya kijiji cha Mazombe – wapangishiwe vyumba ndani ya kijiji cha Mazombe.**
- ii Fomu ya tabibu (Medical Examination Form) iliyojazwa vizuri na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- iii Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia binafsi ya mwanafunzi/mkataba wa kutokukiuka kanuni, taratibu na sheria za shule.
- iv Maelezo ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na kanuni, taratibu na sheria za shule pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa.
- v Cheti cha kuzaliwa – ni muhimu sana.

**TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYAELEWA  
KIKAMILIFU**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAZOMBE**

.....  
**CRISPIN C. NGATUNGA**  
**MKUU WA SHULE**

PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
MAZOMBE SECONDARY SCHOOL  
FOR MEDICAL EXAMINATION

*(To be filled by a Medical Officer for Form one entrants)*

Student's Full name .....

Age ..... Years.....Sex .....

Blood count (red and white) .....

Stool Examination .....

Syphilis and other venereal diseases Test .....

TB test .....

Ears .....

Eye Test .....

Spleen .....

Abdomen .....

Urine .....

Pregnancy (Girls only) .....

ADDITIONAL INFORMATIONS (If any)

Physical defects .....

Chronic disease or Family disease .....

I certify that I have examined the above named student and that he/she is fit/unfit\* to pursue his/her lesson/duties as reached.

Station ..... Signature .....

Designation ..... Date .....

Note: Medical Officer

Please when examining, note any ailment observed.

**This form should be brought to school together with the acceptance form. No pupil will be admitted in absence of this form.**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
SHULE YA SEKONDARI MAZOMBE  
FOMU YA MAKUBALIANO**

**PASSPORT  
SIZE**

**1. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi ..... Mvulana/Msichana\* nimesoma na kuyaelewa maelekezo yaliyotolewa katika fomu ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mazombe. Ninakubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha kwanza mwaka ..... katika shule ya Sekondari Mazombe. Nitatii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za nchi.

**JINA** .....

**SAHIHI** .....

**2. SEHEMU YA MZAZI**

Mimi ..... ninakubali ..... mtoto ..... wangu .....  
..... kujiunga katika shule ya Sekondari Mazombe kidato cha kwanza mwaka ..... Nimesoma na kuelewa maelekezo yote yaliyotolewa katika fomu ya kujiunga. Ninaahidi kumpatia huduma na mahitaji yote yaliyohitajika kama ilivyo katika fomu ya kujiunga. Nitashirikiana na shule katika kuhakikisha mtoto wangu anatekeleza wajibu wake shuleni, jamii na Taifa.

Anwani yangu ya kudumu ni

.....  
.....  
.....  
.....

**Sahihi** .....

**Tarehe** .....

**Simu** .....